# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI TAMBAZA** Barabara ya Umoja wa mataifa, Upanga Magharibi
S.L.P 20576, Simu: +255 784 849 761
DAR-ES-SALAAM. **www.tambaza.sc.tz**

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TAMBAZA KIDATO CHA TANO 2024/25.

**Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi: ________________________________________________________**

Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari **TAMBAZA** kwa mwaka wa masomo **2024/25** tahasusi (Combination) ya ____________________

Shule ya Sekondari Tambaza ipo katika Jiji la DAR ES SALAAM. Usafiri wa daladala unapatikana kupitia barabara ya **UMOJA WA MATAIFA**. Hii ni shule ya mchanganyiko (wavulana na wasichana).

**Shule ya Sekondari TAMBAZA ni shule ya KUTWA(DAY).** Mzazi / Mlezi unashauriwa ukae na mwanafunzi nyumbani na **SIYO** kumpangishia nyumba au Hosteli binafsi ambazo hazina uangalizi wala maadili mema.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ______________ hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ______________ mwisho wa kuripoti ni tarehe ____________

**NB;** Zipo nafasi chache za **BWENI** ndani ya Shule kwa **WANAFUNZI WA KIKE** wanaopangwa na OR-TAMISEMI kujiunga nazo. Hao watapatiwa **FOMU MAALUM** zenye maelekezo kuhusu **BWENI**.

### 1.0. MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

### 1.1. SARE YA SHULE

KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUWA NA SARE KAMILI YA SHULE. HAKIKISHA KUPATA RANGI HALISI NA KUSHONA KUFUATANA NA VIGEZO VYA SHULE.

**a) SARE YA SHULE KWA WAVULANA**

(i) Suruali (2) za “Light Grey”yenye marinda mawili mbele na TURNUP upana chini inchi 16-18 ndefu zinazofika chini ya vifundo vya miguu yenye mfuko mmoja wa ndani nyuma.

(ii) Mashati (2) MEUPE, Tetron mikono mifupi yenye mfuko mmoja - marefu yanayofunika mifuko ya suruali, yasiyobana.

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba (Vyenye Gidamu), kisigino kifupi bapa na visivyochongoka mbele.

(iv) Soksi fupi nyeusi zisizo na urembo wa aina yoyote.

(v) T-SHIRT ya shule (fulana ya GREY yenye kola) yenye nembo pamoja na MOTTO ya Shule

(vi) Mkanda wa ngozi mweusi usio na urembo wa aina yoyote.

(vii) Sweta yenye rangi ya 'dark blue' isiyo na maandishi wala vifungo yenye mshono wa V mbele.

(viii) Nguo za michezo (Track Suit) ya "Light Blue" na viatu vya michezo (Raba nyeupe au nyeusi).

**b) SARE YA SHULE KWA WASICHANA**

(i) Sketi (2) za "Light Grey" zenye **rinda box**(mbele na nyuma), Belt ndogo inchi 1.5 urefu inchi 3 chini ya magoti au ndefu inayofika chini ya vifundo vya miguu.

(ii) Mashati (2) MEUPE, Tetron mikono mifupi yenye mfuko mmoja- marefu, yasiyobana au NUSU KANZU nyeupe ya tetron, hii ifike katika magoti na iwe isiyobana. Itavaliwa pamoja na Juba jeupe ambalo litafunika kifua hadi chini ya kitovu na lifike kwenye viwiko vya mikono.

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba(Vyenye Gidamu) vyenye kisigino kifupi visivyo na urembo.

(iv) Soksi fupi nyeusi zisizo na urembo wa aina yoyote.


(v) T-SHIRT ya shule (fulana ya GREY yenye kola) yenye nembo pamoja na MOTTO ya Shule

(vi) Sweta yenye rangi ya 'dark blue' isiyo na maandishi wala vifungo yenye mshono wa V mbele.

(vii) Nguo za michezo (Track Suit) ya "Light Blue" na viatu vya michezo (Raba nyeupe au nyeusi)..

**NB;** Sare ya Shule itavaliwa VIZURI wakati WOTE Mwanafunzi awapo katika maeneo ya Shule, katika ziara za kielimu na maandamano halali. T-SHIRT ya shule itavaliwa siku za **JUMATANO** na **IJUMAA** tu.

**MICHORO KWA AJILI YA SURUALI NA SKETI YA SHULE**.




## 1.2. MAHITAJI MUHIMU

i) Wanafunzi wote wanapaswa kuleta **REAM MBILI (2)** za karatasi **(A 4)** kwa mwaka**.**

ii) Madaftari 6(COUNTER BOOK QUIRE 3) na manne (4) madogo (MSOMI).

iii) Kifaa cha usafi kulingana na tahasusi aliyochaguliwa (orodha imeambatishwa).

iv) Wanafunzi wanaosoma michepuo ya sayansi na ile ya uchumi wawe na **Scientific Calculator (CASIO Fx991ES)** na **Mathematical Sets**.

v) Wanafunzi wanaosoma somo la Biolojia (PCB&CBG) wanunuliwe **"Dissecting Kit"**

vi) Vitabu vya masomo: inashauriwa kumnunulia mwanafunzi vitabu kulingana na masomo anayosoma- **orodha itapatikana ofisi ya taaluma shuleni.**

Vii) Mwanafunzi mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea anatakiwa awe na KITAMBULISHO CHA NIDA au namba ya NIDA kwa ajili ya kukatiwa BIMA YA AFYA kwa wasiokuwa nazo. Bima ya afya kwa wanafunzi italipiwa 50,400/=(cash) hizi zitakabidhiwa shuleni wakati wa kuripoti.

## 1.3. MICHANGO YA SHULE

| | MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 35,000 |
| 2. | Tahadhari | 5,000 |
| 3. | Nembo ya shule | 5,000 |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000 |
| | **JUMLA** | **50,000** |

Fedha zote za Michango ya Shule zilipwe katika akaunti ya Shule Na. **0150251318000** katika Benki ya **CRDB**.
Jina la akaunti ni **"TAMBAZA SECONDARY SCHOOL"**

**NB:** **"BANK PAY IN SLIP"** iwe na; **Jina kamili la Mwanafunzi**, **Darasa, Mchepuo na Mwaka wa masomo**.
**"Bank Pay in Slip" ILETWE SHULENI WAKATI WA USAJILI.**

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana nchini na ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**A. HESHIMA**

i) Heshima kwa Viongozi, Walimu, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii) Kusimama na kumsalimu Mwalimu, Mzazi au Kiongozi anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

iii) Kutumia LUGHA NZURI ya heshima mahali popote kwa mtu yeyote.

iv) Kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za Viongozi wa NCHI, Nembo ya Taifa (Court of Army), Fedha na Wimbo wa Taifa

v) Kuheshimu ofisi za Shule, ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, mali za umma na mali binafsi zilizopo katika mazingira ya Shule.

vi) Kusimama kwenye mstari wakati wa kupokea huduma. Mwanafunzi akimbie na kuwahi anaposikia wito wa dharura.

vii) Kukubali na kuheshimu tofauti za KIDINI, KISIASA NA KIUTAMADUNI katika jamii. Mwanafunzi haruhusiwi kuhubiri dini, siasa au jambo lolote shuleni. Sala zote zifanyike mahali panapohusika kama vile; Kanisani, Msikitini na katika vipindi vya dini vilivyopangwa kwenye ratiba ya shule.

**B. RATIBA YA SHULE**

viii) Mwanafunzi awepo shuleni saa kumi na mbili na nusu(12.30) asubuhi. Mwanafunzi anatakiwa kukaa darasani muda wote wa vipindi na kutimiza wajibu na kazi alizopewa. Muda wa kutoka ni saa tisa na nusu alasiri (9.30)

**MUHIMU:**

Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya Mwanafunzi

Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.

Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule (Msiba au Ugonjwa).

**C. MIPAKA YA SHULE**

ix) Mwanafunzi aifahamu vizuri mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu kuwepo ndani ya mipaka hiyo au nje ya mipaka hiyo kwa kibali maalum wakati wote. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea/kuingia kwenye nyumba za starehe, vilabu vya pombe na nyumba za kufikia wageni.

**D. USAFI**

Kutunza usafi wa mwili; Nywele fupi njiti ya kiberiti isinase, mkato wa kawaida bila mtindo wowote.

**Mwanafunzi haruhusiwi;** kusuka nywele, kutinda nyusi, kupaka wanja, kupaka rangi za midomo, kuweka dawa/rangi za nywele, kufuga kucha au kuzipaka rangi/hina, kufuga mustachi au ndevu, Kuvaa *bangili, hereni, mikufu, pete* au urembo wowote.

Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya Shule wakati wote unapokuwa katika mazingira ya Shule na katika mikusanyiko maalumu ya kitaifa na kishule. Sare zivaliwe vizuri wakati wote, Shati / T-shirt lichomekewe vizuri ndani ya suruali / sketi. Mwanafunzi atakayevaa sare ya shule isiyokidhi vipimo vilivyoelekezwa na Shule ataadhibiwa na atalazimika kushona / kununua nyingine. Nguo za michezo zitavaliwa siku **maalum** za michezo.

Mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na kutoandika katika kuta za majengo, kutotupa ovyo takataka za aina yoyote darasani au nje ya darasa, kutokatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.

**Mwanafunzi haruhusiwi**; kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo za shule bila ruhusa ya Mwalimu anayehusika na mada ya tangazo hilo.

**D. MAHUDHURIO**

Mwanafunzi ambaye hatahudhuria masomo kwa zaidi ya siku mbili (2) mfululizo kwa sababu yoyote ile, haruhusiwi kuhudhuria masomo mpaka apate kibali kutoka IDARA YA TAALUMA. Vile vile mwanafunzi ambaye hatahudhuria masomo kwa jumla ya siku tano (5) bila taarifa kabla ya Mtihani wowote wa shule, hataruhusiwa kufanya mtihani huo.

Kila mwanafunzi anawajibika **kuhudhuria vipindi vyote** vya masomo ya mchepuo wake pamoja na kipindi cha **DINI**.

**E. SIMU NA VIFAA VYA KI-ELECTRONIKI**

Mwanafunzi **HARUHUSIWI** kumiliki na/au kutumia simu, IPOD au kifaa chochote cha electroniki akiwa shuleni. Mwanafunzi akikamatwa na simu, IPOD au kifaa chochote cha electroniki kisichoruhusiwa ataadhibiwa na kifaa kitachukuliwa na kuharibiwa.

## 2.0. MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE:

1 Makosa ya jinai

2 UTORO kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa.

3 Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo na kuvuruga AMANI NA USALAMA wa Shule au watu.

4 Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,Mwalimu,Mfanyakazi au mtu yeyote.

5 Kupiga na/au kupigana na Mwanafunzi mwenzie, Mwalimu, Mfanyakazi au mtu yeyote.

6 Kufuga ndevu au kusuka nywele.

7 Ulevi au unywaji wa pombe, uvutaji bangi na matumizi ya dawa za kulevya.

8 Uvutaji wa sigara.

9 Kudharau Bendera ya Taifa

10 Kuoa au kuolewa

11 Kupata mimba, Kutoa mimba au Kusababisha mimba ndani au nje ya Shule

12 Kushiriki; matendo ya uhalifu, Siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za Nchi.

13 Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

14 Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 3.0. USAJILI

**Mwanafunzi awasilishe vielelezo / vitu vifuatavyo kwa ajili ya Usajili:**

(i) Fomu ya maelezo (yenye picha) pamoja na mkataba wa Mwanafunzi kuzingatia Sheria na Kanuni za Shule.

(ii) Maelezo ya Mzazi / Mlezi kukiri kukubaliana na; Sheria, Kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule

(iii) "Medical Examination Form" ambayo imejazwa na Mganga/Daktari wa Hospitali ya Serikali

(iv) Nakala (copy) za;

- **a) CHETI CHA KUZALIWA** (Birth Certificate)
- **b) RESULT SLIP** (Form Four NECTA Results)

(v) Ream ya karatasi na vifaa vya usafi alivyopangiwa kulingana na tahasusi (combination) aliyochaguliwa.

# KARIBU SANA SHULENI TAMBAZA

HUSSEIN Z. MAVUMBA

**MKUU WA SHULE**

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa mahututi hivyo mzazi atumepesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-

Mkuu wa Shule 0784-849761

Makamu Mkuu wa Shule 0717-086199

Mwandamizi Taaluma 0715-944261

Mwandamizi Malezi 0713-163188

## UJAZAJI WA FOMU ZA KUJIUNGA NA USAJILI (MUHIMU SANA)

i. TAARIFA **ZOTE** KWENYE FOMU YA USAJILI ZIJAZWE VIZURI KWA USAHIHI
ii. PICHA YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI ANAYEISHI NA MWANAFUNZI NI LAZIMA (PICHA ZIWE ZA NDANI YA MIAKA MIWILI).
iii. TOA NAKALA (PHOTOCOPY) ZA VIAMBATISHO VYOTE VINAVYOHITAJIKA
iv. MWANAFUNZI AVAE SARE (UNIFORM) WAKATI WA USAJILI
v. MWANAFUNZI AKAMILISHE TARATIBU ZOTE ZA USAJILI KABLA YA KUANZA MASOMO
vi. USAJILI KWA WANAFUNZI WOTE HUFANYIKA KUANZIA **SAA MBILI NA NUSU** (2.30) ASUBUHI HADI **SAA TANO NA NUSU** (5.30) ASUBUHI KWA SIKU ZA USAJILI.

***TAFADHALI ZINGATIA SANA MUDA.***

# VIFAA VYA USAFI

Kila mwanafunzi anatakiwa kuleta kifaa cha usafi kulingana na mchepuo aliopangiwa, kama ifuatavyo:

PMCs – **Dawa/Sabuni ya kusafishia Choo (CARE LINE 5lts).**

PCM – **Fagio MBILI laini za ndani (Soft broom 2) NA VIM (1000grm) moja.**

PCB – **Fagio MBILI za mpira za kudekia (Squizer 2) NA ARO (lita moja) moja.**

CBG – **Sabuni ya usafi wa JUMLA (TARMOL 5lts).**

PGM – **Fagio/Brush ya kuondolea BUIBUI ya PLASTIC.**

EGM – **Brush ya kusafishia choo NA kizoleo cha takataka.**

HGE – **Ndoo KUBWA NYEUPE yenye bomba(20lts) moja.**

HGL – **Fyekeo (Slasher) moja AU Ndoo ndogo mbili (lita kumi).**

HKL – **Fagio MBILI ndefu za nje (Street broom-CHELEWA 2).**

BuAcM – **Panga AU REKI moja.**

EBuAc – **Jembe KUBWA moja lenye mpini.**

EBuI – **MKASI wa kukatia majani/maua.**

ECAc – **Kifaa cha kutupia takataka (Dustbin kubwa lita 20 au zaidi).**

- ***Vifaa vya usafi viwe HAVIJATUMIKA (vipya)***
- ***Shule HAIPOKEI PESA TASLIMU kwa ajili ya vifaa vya usafi na ream a karatasi vilivyoagizwa***

# **2024/25**

***ADM NO.________________**

# FOMU YA KUJIANDIKISHA

| PICHA YA MZAZI/MLEZI | PICHA YA MWANAFUNZI |
|---|---|
| | |

**TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (TAARIFA ZIJAZWE KWA HERUFI KUBWA)**

1. Jina kamili la mwanafunzi ______________________________________________
2. Jinsi (Me / Ke) __________ Tarehe ya kuzaliwa ___________________________
3. Wilaya alikozaliwa ______________________ Mkoa ______________________________
4. Uraia ________________________________________
5. Dini _____________________________ Madhehebu ________________________________
6. Mahali unapoishi sasa _________________________________________________
7. Michezo anayoshiriki __________________________________________________
8. Jina la Shule alikomaliza kidato cha nne __________________________________________
9. Namba ya Mtihani kidato cha nne _____________________________
10. Daraja la ufaulu (Division) _________________ Alama za ufaulu (Point) _______________

**TAARIFA ZA MZAZI / MLEZI (ALIYEBANDIKA PICHA)**

11. Jina la Mzazi / Mlezi _________________________________________________
    a) Uhusiano na Mwanafunzi _______________________________________________
    b) Kazi ya Mzazi / Mlezi __________________________________________________
    c) Mahali anapoishi _____________________________________________________
    d) Anuani ya Posta _____________________________________________________
    e) Namba ya simu ya Mzazi / Mlezi ________________________________________
    f) Saini ya Mzazi / Mlezi _______________________

## TAARIFA KUHUSU WAZAZI WA MWANAFUNZI (MZAZI TU SIO MLEZI)

- JINA LA BABA MZAZI ______________________________________________________

  KAZI ANAYOFANYA ________________________ NAMBA YA SIMU ___________________

  MAHALI ANAPOISHI________________________________ SAINI _____________________

- JINA LA MAMA MZAZI _____________________________________________________

  KAZI ANAYOFANYA ________________________ NAMBA YA SIMU ___________________

  MAHALI ANAPOISHI________________________________ SAINI _____________________

  **NB;** Iwapo Mzazi amefariki andika jina kamili na neno AMEFARIKI baada ya jina.

## Ahadi ya Mwanafunzi

Mimi ____________________________________________________ nakubali nafasi niliyopewa ya kidato cha Tano tahasusi (Combination) _______________ mwaka **2023/24.**

Naahidi kutii kikamilifu Sheria na Kanuni zote za Shule wakati wote nitakapokuwa Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Tambaza.

Saini ya Mwanafunzi __________________________ Tarehe ________________________

## Ahadi ya Mzazi / Mlezi (Anayeishi na Mwanafunzi - Aliyebandika picha)

Mimi _______________________________________ ambaye ni ________________ (uhusiano) wa Mwanafunzi ______________________________________ naahidi kushirikiana na waalimu pamoja na uongozi wa Shule katika Malezi na kufuata Sheria, Kanuni na taratibu zote za Shule.

Saini ya Mzazi / Mlezi_________________________ Tarehe__________________________

**KWA MATUMIZI YA OFISI**

**a. Boharia:**

Vifaa alivyoleta; Ream ___________________________________________________

Kifaa cha usafi _________________________________________________________

Saini ________________________ Tarehe ____________________

**b. Mhasibu:**

Nathibitisha kwamba mwanafunzi amelipa malipo kama ifuatavyo:

i) Michango: Tshs. ________________

ii) Risiti namba ___________________________________

iii) Saini ya Mhasibu___________________________ Tarehe___________________

**c. Mwalimu MSAJILI:**

Amepangwa kusoma kidato cha Tano Mkondo wa _____________

Saini ________________________ Tarehe ____________________

# DAR ES SALAAM CITY COUNCIL
# TAMBAZA HIGH SCHOOL

## STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by a **GOVERNMENT MEDICAL OFFICER**

**STUDENT'S NAME** ____________________________________________________

**SEX** ________________________ **AGE** ___________________________________

**CLASS AND COMB** ____________________ **YEAR** ___________________________

Please examine the student named above, Put a tick in either **YES or NO** whichever is applicable and COMMENT on him / her about the following;

| S/N | ITEM / PROBLEM | YES | NO | IF YES EXPLAIN |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SIGHT | | | |
| 2. | HEARING | | | |
| 3. | SPEECH | | | |
| 4. | ASTHMA | | | |
| 5. | BLOOD | | | |
| 6. | T. B | | | |
| 7. | B. P | | | |
| 8. | PREGNANCY for Girls | | | |
| 9. | ANY PHYSICAL DISABILITY | | | |
| 10. | ANY OTHER HEALTH PROBLEM | | | |

I do hereby recommend the said student MEDICALLY **FIT / NOT FIT** for Studentship at **TAMBAZA** High School.

NAME OF THE DOCTOR _______________________________________________

SIGNATURE ________________________________

DATE ________________________ OFFICIAL STAMP _________________________